

## Wizara ya Uchukuzi yachukua hatua kutatua changamoto za usafirishaji

Na Mwandishi Wetu

**S**ERIKALI kupitia Wizara ya Uchukuzi imesema imeanza kuchukua hatua kutatua changamoto zinazokwamisha sekta ya usafirishaji.

Changamoto hizo ni pamoja foleni ya muda mrefu katika mpaka wa Tunduma na wingi wa tozo zikiwemo za matumizi ya barabara zinazotowwa kwa madereva wa Tanzania nchini Zambia.

Hayo yamebainishwa katika Mkutano Mkuu wa Kwanza wa Chama cha Wasafirishaji wa Mizigo kwa Barabara Tanzania (TRFA) uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TRFA, Hussein Wandwi alisema moja ya changamoto kubwa ni tozo za barabara nchini Zambia ambazo zimeongeza gharama za uendeshaji kwa wasafirishaji wa Tanzania.

"Moja ya changamoto kubwa ni tozo mpya za barabara za Zambia. Kama wenzetu wanatoza malori yetu, nasi tunapaswa kuwatoza malori yao," alisema Wandwi.

Alisema pia wasafirishaji wanakabiliwa na changamoto ya tozo kutoka halmashauri na Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri Ardhi (LATRA) ikiwemo kodi ya huduma iliyopunguzwa kutoka asilimia 0.3 hadi asilimia 0.25 ya mauzo ya kila robo mwaka ambayo bado inalalamikiwa na wadau.

Aidha, Wandwi alitoa mwito kwa serikali iangalie upya mfumo wa mawakala wa usafirishaji wasio rasmi ili waweze kusajiliwa na kutambuliwa, sambamba na kusajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kuongeza uwazi na ukusanyaji wa mapato.

Mkurugenzi Msaidizi wa Usafiri wa Barabara katika Wizara ya Uchukuzi, Andrew Magombana alisema serikali imepokea malalamiko kuhusu tozo za Zambia na tayari imeanzisha mazungumzo na Serikali ya Zambia ili kupata ufumbuzi wa kudumu.

Kuhusu foleni katika mpaka wa Tunduma, Magombana alisema serikali za Tanzania na Zambia zinafanya kazi kwa pamoja ili kuhakikisha mpaka huo unakuwa sehemu ya kupita badala ya kuwa sehemu ya kusubiri.

Makamu Mwenyekiti wa TRFA, Sophia Caroline Mansoor alisema chama hicho kitaendelea kushirikiana na serikali ili kutatua changamoto zilizopo.

Mansoor alisisitiza umuhimu wa kuimarisha mazingira ya uwekezaji katika sekta ya usafirishaji kwa kuwa Tanzania ni kitovu cha usafirishaji kwa nchi nyingi kupitia bandari zake.

Mansoor alisema kuboresha mazingira ya biashara katika sekta ya usafirishaji kutachangia katika kukuza uchumi wa nchi na kuvutia uwekezaji zaidi.